NOA BONGO, JENGA MAISHA YAKO

**"Kabumbu Afrika - Ni zaidi ya mchezo"**

**EPISODE ONE: "Ndoto Yangu"**

**MWANDISHI : Chrispin Mwakideu**

**WAHARIRI: Andrea Schmidt, Thelma Mwadzaya**

**Orodha yawahusika Kipindi cha kwanza:**

- Msimulizi

**SCENE ONE: CENTRAL BUSINESS DISTRICT/TAMBARARE CITY**
- Chedede (mume,14 )
- Komora (mume,14 )

**SCENE TWO: AT AUNT LILY'S FLAT.**
- Aunt Lily (mke, 33 )
- Safina (mke,13 )

**SCENE THREE: MAKEMBA RESIDENCE**
- Jonathan ( mume,15 )
- Mhe.Makemba ( mume,55 )

**SCENE FOUR: "SHAH ELECTRONICS SHOP"**
- Mtangazaji habari na michezo / ufunuzi / hitimisho (mke, 25)
- Chedede (mume,14)
- Sauti ya kwanza (mume, 30)

**INTRO:**

1. **SFX: WHISTLE BLOWS LIKE IT WOULD SOUND AT THE START OF A FOOTBALL MATCH**

Nawasalimu nyote, popote mulipo, na nawaalika tena katika makala mapya ya Deutsche Welle ya Noa bongo,jenga maisha yako. Kipenga kimelia tayari kuwaalika katika safari hii ya vipindi kumi ,vitakavyoyaelezea maisha ya watoto watatu tofauti; Chedede- kijana chokoraa, Jonathan- mtoto wa mwanasiasa maarufu na Safina- msichana wa kijijini aliyehamia jijini Tambarare. Kila mmoja ana ndoto ya kuwa mchezaji bora wa soka.Jee watalazimika kufanya kipi kulitimiza lengo hilo?Ili kufahamu mengi baki nasi hadi tamati katika makala hii ya "**Kabumbu Afrika - Ni zaidi ya mchezo"**.Kipindi chetu cha kwanza **"wachezaji watatu, lengo moja"** kinaanzia jijini Tambarare.

**SCENE ONE: CENTRAL BUSINESS DISTRICT/TAMBARARE CITY**

**(CHEDEDE AND KOMORA BEGGING FOR COINS ON THE STREETS)**

2. **SFX: CITY AMBIENCE.COINS JINGLING IN A TIN CAN**

3. **CHEDEDE: (with resignation)**

Nimechoka Komora. Tumeomba tangu asubuhi , tuko hapa na nyuso zetu za kusikitisha, lakini hakuna anayetuonea huruma.. tumepata sarafu mbili tu!

4. **KOMORA:** Swadakta, na hata hizo sarafu mbili pia usisahau yule bibi alizidondosha kwa bahati mbaya. Laa sivyo, tungekuwa bado tuna kikebe kitupu... na waijua vyema maana ya hilo.

5. **KOMORA/CHEDEDE: (in unison)** Njaa tupu!

6. **CHEDEDE:** Mimi nafikiri tungemfuata na kumregeshea vijisenti vyake?, unajuaje? Labda angetutuza ...

7. **KOMORA: (cuts Chedede short, imitating a female voice)** "Asante sana" **(back to his normal voice)** ndivyo angelisema. Asante alafu kisha, ko!ko!ko!, **(imitating the sound of high heels)** huyo akaenda zake. Amka Dede, zinduka! Sisi ni fukara, tunaitwa chokoraa au ombaomba! Wachafu! Alafu unazungumzia uaminifu na huruma? Wewe heri ungekuwa mtumishi wa kanisa, huku mjini hakukufai... **(starts to laugh**)

8. **CHEDEDE: (with a hurtful emotional voice)** Najua unachokusudia.Si sahihi kwa watu kutudharau .Hawajui tulifikaje hapa.

9. **KOMORA: (still laughing)** Siwezi kuwalaumu, sisi wenyewe hatujui tulifikaje hapa kwenye barabara hatari za mji wa Tambarare.

10. **SFX: BALL MADE OF PLASTIC BAGS BEING DRIBBLED ALONG THE GROUND**

11. **CHEDEDE:** Hii ndio sababu nzuri ya kupaondoka hapa**.**Hakuna mwelekeo, hamna maisha hapa. Twende tukacheze mpira angalau tujiliwaze tuyasahau matumbo yetu matupu.

12. **KOMORA:** Una kichaa, Dede? Mpira wa miguu, kabumbu, soka! Yaani unafikiria mpira tu.Huwezi kuzungumza bila kuutaja mpira? Asubuhi, mpira, mchana: kabumbu, si ajabu, unapolalia makaratasi yako huwa unaota kuhusu mpira**.**

13. **CHEDEDE: (unconcerned)** Kwahiyo tunaandamana au?

14. **KOMORA:** Yaani kumbe hukunisikia nilichokisema? (**shouts)** la! Sitoi guu langu hapa, Dede! Nahitaji pesa za chakula**.**Wewe nenda kacheze huo mpira wako, lakini jioni usije kuniomba mkate wala supu ya maharagwe.

15. **CHEDEDE:** Jee unafahamu mshahara anaoupata mchezaji bora wa soka hii leo? Hata sielewi kwanini nakuelezea yote haya. Tuonane tena baadaye basi, maskani yetu,muda ule ule.

16. **SFX: CITY AMBIENCE. COINS JINGLING**

**17. NARRATOR:**

Dede, kama Komora alivyopenda kumuita,alienda zake, akiwa mkononi mwake amebeba hazina na tumaini lake – mpira wa makaratasi alioutengeneza kwa kutumia mifuko ya plastiki aliyoiokota jaani na akaufunga kwa kamba za makonge. Katika upande mwengine wa jiji, Safina,mwenye umri wa miaka 13 ndio mwanzo amewasili kwa shangazi Lily na mizigo yake. Kwanini yuko hapa? Ni yapi yanamsubiri jijini?Hebu tuyapeleleze.

**SCENE TWO: AT AUNT LILY'S FLAT**

**(SAFINA AT HER AUNTS HOUSE, MUSIC PLAYING LOUDLY)**

**18. SFX: KNOCKING ON DOOR.**

**19. SHANGAZI LILY: ( From inside)** Subiri kidogo !

**20. SFX: SEVERAL BOLTS AND NUTS BEING UNLOCKED**

**21. SHANGAZI LILY:** Enhe, nikusaidie vipi, msichana?

**22. SAFINA: (surprised by her aunts reaction)** Shangazi Lily? Ni mimi, Safina! Ulikuwa unanisubiri niwasili, sivyo?

**23. SHANGAZI LILY:** Safina! Mungu wangu umekuwa kweli? Nisingekutambua huko barabarani. Karibu, ingia, ingia ndani!

**24. SFX: SAME NUMBER OF BOLTS BEING LOCKED**

**25. SAFINA:** Mbona unafunga makufuli na tumbuu nyingi.Kijijini tunafunga na kufuli moja tu...

**26. SHANGAZI LILY:** Karibu jiji la Tambarare! Huku, kuna wezi wa kuvunja majumba haswa, kwa hivyo, makufuli yakiwa mengi inakuwa bora zaidi. Enhe, wazazi wako wanaendeleaje? Dadangu, mamako hana neno?

**27. SAFINA:** Hana neno, wote wamekusalimu. Kabla sijasahau,mama alinipa barua aliyokuandikia. Shangazi, kila mtu shamba yuwaamini kuwa wewe ni tajiri, lakini**... (hesitates)** naona kitanda pekee hapa kwako, na viti viwili... na... kiredio...

**28. SHANGAZI LILY: (not amused)** Safina! Ndio mwanzo umefika na una kauli za ajabu… sidhani kama tutaelewana... hebu niione hiyo barua...

**29. SFX:LETTER BEING RIPPED OPEN**

**30. NARRATOR**

Wakati Shangazi Lily anapoifungua barua yake, hatua chache kutokea hapo kuna mtaa wa kifahari wanakoishi mabwanyenye wa jijini Tambarare. Na hapo Jonathan, mwenye miaka 15, mtoto wa kiume wa mwanasiasa maarufu, mheshimiwa Makemba, amejilaza kochini akicheza toleo jipya la kandanda ya kisasa kwenye

kompyuta.

**SCENE THREE: MAKEMBA'S RESIDENCE**

31. **SFX: SOUNDS OF BEEPING FROM A COMPUTER GAME**

32. **JONATHAN: (Very excited)** Ndio!... Mchenge huyo, sawa, piga... mkwaju! Baoooo! **(cheering wildly)**

33. **HON. MAKEMBA: (shouts from outside)** Jonathan! Jonathan!

34. **JONATHAN:** Baba, hutoamini, njoo utazame nikiweka marudio. Nimeishinda timu bora ulimwenguni. Mimi ni bingwa! nimewashinda! **(starts to celebrate with victory chant or song)**

35. **HON. MAKEMBA:** Jonathan, huo ni mchezo wa kompyuta tu. Soka haswa inachezwa katika uwanja wa mpira, ukitumia miguu, kichwa, kifua na magoti. Sio kwa vidole viwili kwenye kompyuta. Ukitaka kuwa mchezaji bora, ni lazima uongeze juhudi.

36. **JONATHAN:** Kwahio nifanye kipi baba?Niko tayari kufanya lolote kukufurahisha. Wewe ni waziri wa michezo wa zamani,lazima nifuate nyayo zako pia.

**37. HON.MAKEMBA: (Contemplating)** Hmm... Jonathan, naiona bidii yako. Pengine nikueleze hili. Kuna tetesi bungeni kuwa mchezaji mmoja maarufu atakuja kuanzisha kliniki ya soka humu nchini.Timu itakayoteuliwa itakwenda Ulaya kushiriki kwenye michuano.Nataka wewe uwe mmoja ya wachezaji hao. Nitafanya kila niwezalo uchaguliwe. Sasa. Twende nje tukacheze ili uanze maandalizi haraka.

**38. JONATHAN: (excited)** Baba! Hizo ni habari njema! Huyo mchezaji ni nani? Na itakuwa lini? **(voices fading away)** unaamini ntaweza kushiriki?

**39. NARRATOR:**

Makemba na mwananawe walienda nje kucheza mpira, Chedede naye aliwasili katika duka la "Shah Electronic" ili atazame kipindi chake anachokipenda, habari za michezo za mchana. Halikuwa jambo rahisi kwanikulijaa pomoni na ilimlazimu kila mmoja kuminyana ndipo upate nafasi ya kutazama. Kwa bahati nzuri, Chedede alikuwa amesimama mahali pazuri.Tujiunge nao tusikie kinachoendelea...

**SCENE FOUR: "SHAH ELECTRONIC SHOP"**

**40. SFX: CROWD VOICES/MURMURS**

**(Unusual silence as the news report begins on TV)**

**41. TV SPORTS ANCHOR:** Hamjambo watazamaji, na karibuni katika habari zetu za michezo. Tunaanza na ligi ya kitaifa ya soka.Timu ya soka ya Tambarare, waliochukuwa taji mwaka jana, walitoka bila kwa bila na mahasimu wao Mitobwe Wanderers. Katika mechi nyengine…....

**(voice fades out)**
**(crowd starts to push and shove with murmurs and squabbles)**

**42. CHEDEDE: (firmly** Usinisukume! nilikuwa wa kwanza kufika hapa!

**43. SAUTI 1: (Arrogantly)** Rudi mapipani ulikotoka,chokoraa wewe!

**44. CHEDEDE:** Siondoki! Hii runinga si yako! Ala!

**45. VOICE 1:** Watoto kama nyinyi munafaa mushikwe, mutiwe ndani na muadhibiwe sawasawa. Bila shaka hamukufunzwa na wazazi wenu....

**46. CHEDEDE: (angrily)** Usiwataje wazazi wangu, huwajui, sawa?

**47. SAUTI 1: (Shocked and scared by Chedede's reaction)**

Sawa. Tuendelee kutizama habari basi.

**KW ENDE POSSIBILITY TO SHORTEN HERE**

**48. TV SPORTS ANCHOR:Ha**timaye, katika habari zetu nyengine za michezo, habari nzuri kwa vijana wetu. Ukiwa kijana aliye na umri kati ya miaka 12 na 16,mkaazi wa hapa Tambarare na unaipenda soka, basi kuna nafasi ya kujitokeza ,na kushiriki katika kliniki ya soka itakayoandaliwa na mchezaji mahiri ambaye jina lake kwa sasa bado tunalibana.Timu itakayoteuliwa itashiriki katika ziara rasmi ya barani Ulaya maarufu "Goli la amani" kama njia ya kuzipa msukumo juhudi za kudumisha amani na maridhiano hapa nchini. Tutawapa maelezo zaidi yatakapotufikia kituoni. Mwisho wa habari zetu za michezo kwa sasa. Endelea kuwa nasi.

**49. CHEDEDE: (very excited)** Siamini! Hii ndio fursa yangu…! **(calls out)** Komoraaaa! Komoraaa!

**OUTRO:**

**50. NARRATOR:** Sauti hiyo ya Chedede, iliyojaa tumaini,na jitihada iliyosikika kwenye barabara za mji wa Tambarare,ndiyo inayotuhitimishia kipindi chetu cha kwanza **"Kabumbu Afrika - Ni zaidi ya mchezo!"** Komora atazichukulia vipi habari hizi za kliniki ya soka?Jonathan pia yuko kwenye msururu huo wa kuwa mshiriki katika kinyang'anyiro cha uteuzi, akisaidiwa na babake aliye mwanasiasa maarufu,mambo yatakuwaje?Kumbuka kuwa shangazi Lily ameifungua barua aliyoandikiwa na mamake Safina, inasema nini? Kwa haya na mengine mengi jiunge nasi katika kipindi kijacho.Ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki, au chengine katika makala ya noa bongo,jenga maisha yako, tembelea kurasa za tovuti zetu www.dw-world.de/lbe. Mpaka wakati huo. Kwa heri!